HABARI KITAIFA



Treni ya SGR ikiwa katika safari zake za kawaida. **PICHA: MAKTABA**

HOTUBA

# Uchukuzi sasa dhahabu ya uchumi wa Tanzania

**Na Rehema Matowo,** DODOMA

WIZARA ya Uchukuzi imeomba kuidhinishiwa bajeti ya Sh trilioni 2.87 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele nane ikiwamo miradi mikubwa ya kimkakati ya reli ya kisasa ya SGR, maendeleo ya bandari, viwanja vya ndege na huduma za usafirishaji nchini.

Akiwasilisha bungeni mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo jana, kwa Mwaka wa Fedha 2026-2027 Waziri wa Uchukuzi Profesa Makame Mbarawa alisema kati ya fedha hizo, Sh trilioni 2.746 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Sh bilioni 126.04 ni matumizi ya kawaida.

Alitaja vipaumbele vitakavyo tekelezwa kuwa ni kuendelea na ujenzi pamoja na uendeshaji wa reli ya kisasa ya SGR, ukarabati wa reli za MGR na TAZARA, kuboresha miundombinu ya bandari na kuimarisha usafiri wa anga.

Vipaumbele vingine ni kuendelea na ujenzi wa meli pamoja na kuboresha huduma za hali ya hewa,kuboresha usalama na udhibiti wa huduma za uchukuzi pamoja na kuendeleza vyuo vya mafunzo vya kisekta.

Kuhusu mafanikio, Waziri Mbarawa alisema uwekezaji uliofanywa katika reli ya kisasa ya SGR umeanza kuzaa matunda baada ya mradi huo kuingiza zaidi ya Sh bilioni 169 kwa kipindi cha chini ya miaka miwili huku Shirika la Reli Tanzania (TRC) likianza rasmi kujiendesha bila ruzuku ya mishahara kutoka serikalini.

Aidha, zaidi ya abiria milioni 2.51 wamesafirishwa kupitia reli hiyo kati ya Julai 2025 na Machi 2026 huku mizigo zaidi ya tani 102,000 ikisafirishwa.

Waziri Mbarawa alisema katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 Sh bilioni 82.77 zimekusanywa kutokana na usafirishaji wa abiria kati ya Dar es Salaam na Dodoma

Alisema tangu kuanza kwa safari za reli hiyo mwezi Juni 2024 hadi Machi 2026, serikali imekusanya jumla ya Sh bilioni 169.37 kutokana na huduma za reli ya SGR huku huduma za usafirishaji zikiendelea kuimarika siku hadi siku.

"Kutokana na kuongezeka kwa mapato ya TRC, kuanzia Januari 2026 shirika limeanza kujiendesha bila ruzuku ya mishahara kutoka serikalini," alisema Waziri Mbarawa.

Alisema kabla ya hatua hiyo, serikali ilikuwa ikitoa wastani wa Sh bilioni 12.92 kila mwaka kwa ajili ya kugharamia mishahara ya shirika hilo.

Katika hatua nyingine, Waziri Mbarawa alisema serikali imefanikiwa kupata mkopo wa dola za Marekani bilioni 1.277 kwa ajili ya kukamilisha baadhi ya vipande vya reli ya SGR vilivyokuwa vinakabiliwa na changamoto za utekelezaji.

Alisema katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 serikali itaendelea na ujenzi wa vipande mbalimbali vya reli hiyo pamoja na ukarabati wa reli za zamani za MGR na TAZARA ili kuongeza ufanisi wa usafirishaji nchini na katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Aidha alisema serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa treni ya mijini katika Jiji la Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza changamoto ya msongamano wa magari.

Mbali na mafanikio ya reli, Profesa Mbarawa alisema sekta ya uchukuzi imeendelea kufanya vizuri katika maeneo mbalimbali ikiwamo bandari, usafiri wa anga na usafiri wa majini.

Katika sekta ya bandari, alisema Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) imeongeza kiwango cha shehena inayohudumiwa kutokana na maboresho makubwa ya miundombinu na huduma.

Alisema katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, TPA ilihudumia tani milioni 29.66 za shehena ikilinganishwa na tani milioni 23.18 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita, sawa na ongezeko la asilimia 27.96.

Aidha alisema shehena ya mizigo inayosafirishwa kwenda nchi jirani imeongezeka hadi kufikia tani milioni 10.93 kutoka tani milioni 8.24 mwaka uliopita.

Profesa Mbarawa alisema serikali pia imeanza maandalizi ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa Bandari ya Bagamoyo utakaohusisha ujenzi wa gati lenye urefu wa kilomita 1.32 pamoja na miundombinu ya kisasa ya kuhudumia meli kubwa aina ya Megamax.

Alisema serikali kupitia TPA inaendelea pia na ujenzi wa matenki 15 ya kuhifadhi mafuta yenye uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 378,000 ambapo mradi huo umefikia asilimia 42 na unatarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu.

Profesa Mbarawa alisema ushirikiano kati ya serikali na kampuni ya DP World umeongeza ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema kutokana na ushirikiano huo, shehena inayohudumiwa bandarini imeongezeka kutoka tani milioni 16.27 mwaka 2020/21 hadi tani milioni 27.76 mwaka 2024/25.

Aidha alisema muda wa kuhudumia meli bandarini umepungua kutoka wastani wa siku 10 hadi siku tatu huku muda wa kusubiri nangani ukishuka kutoka siku 46 hadi siku saba.

Mafanikio mengine ni kupungua kwa gharama za uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kutoka Sh. bilioni 652.83 mwaka 2023/24 hadi Sh.bilioni 308.95 mwaka 2024/25

**Usafiri wa Anga**

Katika sekta ya usafiri wa anga, Waziri Mbarawa alisema serikali imeendelea kuifufua Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ambapo idadi ya ndege imeongezeka kutoka ndege moja mwaka 2016 hadi ndege 16 mwaka 2026.

Alisema idadi ya abiria imeongezeka kutoka abiria 107,166 mwaka 2016/17 hadi zaidi ya abiria milioni 1.17 mwaka 2024/25 huku mapato yakiongezeka kutoka Sh bilioni 23 hadi Sh bilioni 595.7.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, ATCL ilisafirisha abiria 1,072,528 sawa na ongezeko la asilimia 22.38 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka uliopita.

Alisema serikali itaendelea kuboresha viwanja vya ndege vya Mwanza, Arusha, Musoma, Moshi, Kagera pamoja na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA).

Aidha alisema serikali imepanga kukipandisha hadhi Kiwanja cha Ndege cha Mwanza kuwa kiwanja cha kimataifa ambapo tayari upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina wa mradi huo umekamilika.

**Usafiri wa Majini**

Katika sekta ya usafiri majini, Profesa Mbarawa alisema serikali imekamilisha ujenzi wa meli ya MV New Mwanza katika Ziwa Victoria pamoja na kukamilisha ujenzi wa meli nne za mizigo katika Ziwa Tanganyika.

Alisema ukarabati wa meli ya MV Liemba umefikia asilimia 64 huku maandalizi ya ujenzi wa meli mpya ya mizigo katika Ziwa Victoria yakiendelea.

Kwa upande wa reli ya TAZARA, alisema serikali za Tanzania na Zambia zimesaini mkataba wa kufufua reli hiyo kupitia kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation ambayo itawekeza dola bilioni 1.4 sawa na Sh trilioni 3.6.

Alisema mradi huo unatarajiwa kuongeza uwezo wa kusafirisha mizigo hadi tani milioni 2.4 kwa mwaka pamoja na kuzalisha ajira mpya 100,000.

Katika sekta ya usafiri ardhini, Waziri Mbarawa alisema LATRA imetoa leseni 388,715 za usafirishaji huku mabasi 13,843 yakiunganishwa kwenye mfumo wa ufuatiliaji wa VTS kwa ajili ya kuongeza usalama wa safari.

Aidha alisema zaidi ya abiria milioni 21 walitumia mfumo wa tiketi mtandao kununua tiketi za mabasi hadi kufikia Machi 2026.

Profesa Mbarawa alisema kutokana na miradi mbalimbali ya uchukuzi inayoendelea nchini, sekta hiyo imezalisha ajira 198,480 kupitia shughuli za ujenzi wa miundombinu pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali za usafirishaji.

**Miradi itakayotekelezwa**

Waziri Mbarawa alisema katika Mwaka wa Fedha 2026/27 serikali imelenga kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ambayo ni pamoja na Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam (DMGP).

Miradi mingine ni ile ya kuboresha usafiri wa anga na hali ya hewa nchini, ambapo serikali imelenga kununua ndege , kuimarisha kampuni ya ATCL, kujenga Chuo cha Usafiri wa Anga pamoja na kujenga, kukarabati na kuboesha viwanja vya ndege .

Alisema Wizara hiyo pia itaendeleza miundombinu ya reli pamoja na uboreshaji wa vyuo vya mafunzo ya kisekta.

za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi mama na babalishe

**Nasisitiza kushauri kwamba kupandisha kwa nauli kuendane na kukomesha ujazaji wa abiria kupita kiasi na adha ya abiria kusimama kama mizigo.**



Na JUMANNE GUDE

# Nauli mpya ziendane na huduma bora

HIVI karibuni kumekuwa na ongezeko la nauli mpya za mabasi ya masafa marefu, mabasi ya mijini 'daladala' teksi na pikipiki mtandao.

Kupanda kwa nauli hizo kunaelezwa kuwa, kunatokana na kupanda kwa gharama za uendeshaji wa shughuli za usafirishaji kupitia vyombo vya moto.

Wakati wasafirishaji wakijenga hoja kuwa kuongezeka kwa gharama za uendeshaji ndicho kinachochochea kupanda kwa gharama, abiria kwa upande wao wanatarajia kuona thamani ya fedha wanazolipa inaendandana huduma waipatayo.

Hoja yangu imejikita katika usafiri wa daladala ambao ni uti wa mgongo kwa uchumi wa miji yetu, lakini huduma hiyo imegubikwa na kero ikiwemo ya uhafifu wa usafi, lugha chafu, ukiukwaji wa utaratibu na sheria zikiwemo za usalama barabarani.

**Kwa upande wa wamiliki wa vyombo hivyo, wana wajibu wa kuboresha vyombo vyao ikiwemo kuboresha viti, sakafu na vioo vyenye nyufa, kwa kuwa daladala chafu ni kiota cha magonjwa na kero kwa mlipa nauli.**

Ni matarajio ya abiria kuwa, nauli mpya zinazotarajiwa kuanza karibuni, zitachochea kuondoa kero hizi na kushuhudia huduma zinaendana na thamani ya fedha.

Madereva na makondakta wa daladala ni mabalozi kwa watumiaji wa usafiri wa umma, hivyo wanatakiwa kuwa wasafi kuanzia mwili hadi mavazi yao, wanapovaa nguo chafu ikiwamo kutoa harufu mbaya wanajishushia hadhi wao wenyewe na biashara zao.

Kupanda kwa nauli kunapaswa kuendane na kuboreshwa huduma zao, wanapaswa kuacha kutoa lugha za kashfa, kusukuma abiria au kutoheshimu makundi maalumu kama wazee na walemavu.

Kwa upande wa wamiliki wa vyombo hivyo, wana wajibu wa kuboresha vyombo vyao ikiwemo kuboresha viti, sakafu na vioo vyenye nyufa, kwa kuwa daladala chafu ni kiota cha magonjwa na kero kwa mlipa nauli.

Kwa upande wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), inapaswa kwenda mbali zaidi ya kupanga nauli kwa kuanzisha mfumo ambapo abiria wanaweza kutoa maoni kwa njia ya ujumbe mfupi (SMS) au App kuhusu hali ya gari au tabia mbaya za madereva na makondakta wa daladala.

Mfumo huo utasaidia kutambua gari lenye malalamiko mengi kunyang'anywa leseni ya usafirishaji.

Kudhibiti ruti kwa kuhakikisha daladala zinatimiza ruti zao na kuzuia tabia ya kukata ruti ambayo huwalazimisha abiria kulipa nauli mara mbili kwa safari moja.

Ushauri kwa Kikosi cha Usalama Barabarani, kihakikishe sheria na kanuni za usalama barabarni zinafuatwa bila upendeleo, ukiwemo ukaguzi wa ubora wa magari, daladala chakavu lisiruhusiwe kubeba abiria .

Nasisitiza kushauri kwamba kupandisha kwa nauli kuendane na kukomesha ujazaji wa abiria kupita kiasi na adha ya abiria kusimama kama mizigo.

Hilo likifanyika litaongeza heshima kwa abiria na usalama pindi ajali inapotokea.

Usafiri wa umma unapaswa kuwa na hadhi, hivyo kupanda kwa nauli ni fursa kwa wamiliki kuwekeza kwenye vyombo vipya au kuyatengeza magari yanayotoa huduma yawe na viwango bora na wahudumu wasafi.

LATRA na Polisi kuhakikisha mnasimamia kwa weledi haki za abiria.

## TULIKOTOKA



WANANCHI wakiwa na Mwenge wa Uhuru mkoani Shinyanga. Hiyo ilikuwa Juni, 1974.

